**TANGAZO KWA UMMA**

**KANUNI ZA USIMAMIZI WA MADUKA YA KUUZA NA KUNUNUA FEDHA ZA KIGENI**

Benki Kuu ya Tanzania inapenda kutoa taarifa kwa umma kuwa imetoa kanuni mpya zinazohusu uendeshaji wa biashara ya maduka ya fedha za kigeni (Bureaux de Change Regulations) za mwaka 2008. Kanuni hizo zilichapishwa kwenye Gazeti la Serikali (Government Gazette) No. 88 la tarehe 20 Juni, 2008 na kuanza kutumika kuanzia tarehe 01/07/2008.

Pamoja na maeneo mengine mengi yaliyoainishwa katika kanuni mpya zinazohusu biashara ya maduka ya fedha za kigeni, Benki Kuu inapenda kusisitiza kwa umma vipengele vifuatavyo vya Kanuni hizo:-

1. Kanuni ya 5(1) inayotaka biashara ya maduka ya fedha kusajiliwa katika mfumo wa kampuni.

2. Kanuni ya 5(3) inayotaka uongozi na umiliki wa maduka ya fedha za kigeni kuwa ni raia wa Tanzania.

3. Kanuni ya 6(1) inayotaka maduka ya fedha za kigeni kuanza biashara yakiwa na mtaji usiopungua shillingi milioni arobaini (TZS 40,000,000).

4. Kanuni ya 11 inayotaka shughuli zote katika maduka ya fedha za kigeni kutumia mifumo ya elektroniki itakayoweza kutoa stakabadhi zinazoonyesha muda kwa kila mauzo na manunuzi ya fedha za kigeni.

5. **Kanuni ya 14(1)(a)-(c) inayoeleza mazingira ambayo leseni ya kufanya biashara ya duka la fedha za kigeni inaweza kufutwa ikiwemo kushindwa kuanza biashara katika muda wa miezi sita kutoka leseni inapotolewa bila ruhusa ya maandishi ya Benki Kuu, kufanya biashara bila kuzingatia mipaka ya shughuli zilizoruhusiwa katika leseni na inapotokea kampuni husika kufilisika.**

6. Kanuni ya 15(b) inayoyataka maduka ya fedha za kigeni kuweka tangazo linalowataka wateja kudai na kupewa stakabadhi kwa mauzo na manunuzi yoyote ya fedha za kigeni.

7. Kanuni ya15(c) inayotaka maduka ya fedha za kigeni kutoa stakabadhi kwa kila mauzo au manunuzi ya fedha za kigeni. Stakabadhi inatakiwa ionyeshe muda wa mauzo au manunuzi na wateja wanatakiwa kuonyesha utambulisho wao.

   **Benki Kuu inasisitiza ni haki ya mteja kudai na kupokea stakabadhi kwa kila mauzo au manunuzi ya fedha za kigeni kutoka katika duka la fedha za kigeni. Aidha, ni kosa kwa upande wa duka la fedha za kigeni kutokutoa stakabadhi kwa kila mauzo au manunuzi ya fedha za kigeni. Benki Kuu pia inawataka wateja wanaouza au kununua fedha za kigeni, wawe na vitambulisho vyenye kuonyesha jina kamili na namba ya kitambulisho ili kuweza kupata huduma katika duka la fedha za kigeni. Wateja wote wanahimizwa kufuata kanuni hii kutimiza matakwa ya sheria na kuepuka usumbufu usio wa lazima.**

8. Kwa mujibu wa kanuni ya 15(d), maduka ya fedha za kigeni yanatakiwa kuhifadhi kivuli cha kitambulisho na kielelezo cha sababu ya maombi ya kuuziwa (supporting documents) fedha za kigeni yanayozidi dola za Kimarekani Elfu Mbili ($ 2,000) au kiwango kinachofanana na hicho, kama fedha zinazouzwa si dola za Kimarekani.

**Benki Kuu inasisitiza kwamba sheria inawataka wateja kutoa vitambulisho vyao na vielelezo pamoja na sababu ya kununua fedha za kigeni wanapotaka kununua fedha hizo, pale ambapo kiwango kinachotakiwa kinapozidi dola za Kimarekani elfu mbili ($ 2,000) pamoja na kuwezesha upatikanaji wa kumbukumbu sahihi. Wateja wote wa maduka ya fedha za kigeni wanatakiwa kutimiza masharti haya ya sheria ili kuepuka usumbufu .**

9. Kanuni ya 16 inaeleza kuwa biashara pekee inayoruhusiwa kisheria kufanywa na maduka ya fedha za kigeni ni ya kuuza na kununua fedha za kigeni kwa mtindo wa papo kwa hapo (Spot buy and sale basis). Kwa hiyo umma unajulishwa kuwa maduka ya kubadilisha fedha za kigeni hayaruhusiwi kufanya biashara zifuatazo:-

   i) Kutuma fedha nje ya nchi au kupokea fedha kutoka nje ya nchi (Money Transfers)

   ii) Kuchukua fedha za kigeni kwa ajili ya kutoa shilingi za ki-tanzania baadaye **au kinyume chake**.

   **Umma unakumbushwa kuwa taasisi zinazoruhusiwa kutuma fedha nje ya nchi na kupokea fedha kutoka nje ya nchi ni mabenki na taasisi za fedha pekee. Duka lolote la fedha za kigeni linalojihusisha na biashara ya kutuma fedha nje ya nchi au kupokea fedha kutoka nje ya nchi linakiuka sheria na hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa yale yatakayobainika kufanya hivyo ikiwa ni pamoja na kufutiwa kibali cha kufanya biashara.**
   **Wananchi wanahimizwa kutoa taarifa ya maduka hayo Benki Kuu na vyombo vya sheria.**

10. Kanuni ya 19 na 22 zinaelekeza maduka ya fedha za kigeni kutouza fedha za kigeni kwa kiwango kinachozidi Dola za Kimarekani Elfu Kumi ($10,000) au kwa kiwango kinachofanana na hicho, kama fedha inayouzwa si dola ya kimarekani.

11. Kanuni ya 22 (1) na (2) inayataka maduka ya fedha za kigeni kuhifadhi kivuli cha tiketi na shahada ya kusafiria kama mauzo yanayofanyika ni kwa ajili ya matumizi ya safari kwa fedha inayozidi Dola za Kimarekani Elfu mbili ($ 2000) au kwa kiwango kinachofanana na hicho, kama fedha inayouzwa si dola ya kimarekani.

**Kwa tangazo hili umma unasisitizwa kuzingatia maelekezo ya kanuni hizo wanaponunua au wanapouza fedha za kigeni kwenye maduka ya kubadilisha fedha za kigeni.**

Taarifa zaidi ya kanuni zinazosimamia maduka ya kubadilisha fedha za kigeni zinapatikana kwenye tovuti ya Benki Kuu, www.bot.tz.org

**BENKI KUU YA TANZANIA**
**19 JANUARI 2010**